



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA HALMASHAURI YA WILAYA YA UYUI



16/04/2024

YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Uyui anawatangazia wananchi wote wenye sifa kuomba nafasi ya kazi ya Mkatoba kama ifuatavyo:-

1.0. AFISA UVUVI MSAIDIZI – NAFASI (2)

SIFA ZA MWOMBAJI:

- Awe na elimu ya Kidato cha Nne (Form IV) au Sita (VI) aliyehitimu Mafunzo ya Afisa ya Uvuvi kutoka chuo cha Mbegani au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali:-

1.1. KAZI ZA KUFANYA:

- (i) Kutekeleza Sera ya Uvuvi
- (ii) Uhifadhi wa samaki na viumbe wengine wa majini na mazingira yao
- (iii) Kuratibu na kusimamia uhifadhi wa mazingira
- (iv) Kuendeleza uvuvi endelevu wa samaki na viumbe wengine wa maziwa, mito mabwawa na malambo.
- (v) Kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu uvuvi bora, utengenezaji wa uhifadhi bora wa samaki pamoja na ufugaji wa samaki na viumbe wengine wa majini.
- (vi) Kutoa leseni za uvuvi na vyombo vya uvuvi katika mfumo wa TAUSI
- (vii) Kuendesha mafunzo ya taaluma ya uvuvi
- (viii) Kusimamia utekelezaji wa sheria za uvuvi
- (ix) Kusimamia ukusanyaji wa Takwimu za Uvuvi pamoja na maduhuli
- (x) Kuratibu shughuli za utafiti wa uvuvi
- (xi) Kukagua ubora wa samaki na mazao ya uvuvi na kuweka viwango vya kitaifa.

MSHAHARA:

- Malipo yatalipwa kulingana na asilimia za makusanyo

MASHARTI YA JUMLA

- a) Waombaji wawe Watanzania wenye umri kuanzia Miaka 18 na usiozidi miaka 45
- b) Muombaji awe tayari kufanya kazi sehemu yoyote katika Halmashauri ya Wilaya ya Uyui
- c) Maombi yote yaandikwe kwa mkono na yaambatishwe na picha moja (passport size), nakala za vyeti vilivyothibitishwa (certified) na Wakili au Mwanasheria anayetambulika na serikali.
 - Cheti cha Shahada/Stashahada ya Juu/ Stashahada/ Astashahada
 - Cheti cha Kidato cha Nne au Sita
 - Cheti cha Kuzaliwa
- d) Waombaji waambatishe taarifa binafsi yani Curricullium Vitae (CV) zikiwa na anwani ya posta na namba za simu.
- e) Waombaji waliosoma nje ya nchi waambatishe ulinganisho (equivalence) kutoka TCU, NECTA au NACTE.
- f) Testimonials, provisional, results na statements za aina yoyote **hazitakubaliwa**
- g) Watakao wasilisha taarifa na sifa za kugushi wakibainika watachukuliwa hatua kali za Kisheria.
- h) Mwisho wa Kuwasilisha maombi ni tarehe **30, Aprili, 2024 Saa 9.30 Alasiri**. Watakaokidhi vigezo na kuchaguliwa kwa ajili ya usaili watajulishwa.

NOTE: Maombi yote yatumwe kwa anwani:-

**MKURUGENZI MTENDAJI (W),
HALMASHAURI YA WILAYA YA UYUI,
S.L.P 610,
TABORA.**


Leokadia G. Humera
Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,
UYUI

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
2 